# KOZI YA KUIJUA BIBLIA

## SEHEMU YA III
## AGANO JIPYA

*(Uchapaji wa kitabu hiki kwa ajili ya matumizi ya binafsi au kanisa unaruhusiwa. Kunakili kwa aina nyingine, kama kwa ajili ya usambazaji, kwa makusudi ya kutangaza, au kuuza, hairuhusiwi.)*

**Kuijua Biblia, Sehemu ya III Agano la Jipya**

By Rosemary P. Nelsen
540 Fairview Avenue, Ripon, WI 54971
rosemarypricenelsen@gmail.com

Bachelor of Science: Education
University of Wisconsin, Oshkosh, WI. Spring, 1972

Elementary Teacher, Washburn, WI, 1972-1977

14 graduate credits from Columbia Graduate School of Bible and Missions, Columbia, S.C., Fall, 1977

Newspaper Reporter/Bureau Chief, Oshkosh Northwestern
Berlin and Ripon Bureaus, 1978-1996

Majukumu mbali mbali ya kazi katika Kanisa ikiwa pamoja na Mwenyekiti wa Elimu ya Kikristo, Mwenyekiti wa Huduma ya wanawake, Mwenyekiti wa Maombi na mara kwa mara Kiongozi wa Masomo ya Biblia, Mwalimu wa Shule ya Jumapili nk.
Kwa kipindi cha cha 1972 mpaka wakati wa sasa

---

**Kimehaririwa na**
Lois E. Gloyd
421 E. Jackson Street, Ripon, WI 54971
legloyd@gmail.com

Associate Degree: Computer Technology 1991
Moraine Park Technical College
Fond du Lac, WI

Aliajiriwa katika Lutheran Homes za Oshkosh 1991 – 2015

Alishakuwa na machapisho katika:
*Country* Magazine
Feb/March 1999
*GreenPrints* Magazine
Spring 2005 and Autumn 2013
*Upper Room* Devotional Guide
July/Aug 2002 and March/April 2010

Mwanzilishi mwenza wa **Sweeter than Honey Ministries** mwaka 2012
Misheni yetu ni kufundisha mambo ya msingi ya Biblia pamoja na Neno Lake, ambalo litahamasisha ukuaji katika Biblia kwa njia ya "kufanywa upya nia zetu" ambako kutatuongoza katika kupima na kuthibitisha "mapenzi ya Mungu yaliyo makamilifu" katika maisha yetu.
*"Mausia yako ni matamu sana kwangu, Kupita asali kinywani mwangu."*
*Zab. 119:103 NIV*

Kozi hii imeandikwa kwa namna inayoruhusu mwanafunzi kuona ile picha kubwa na kuiainisha katika vipengele vilivyo rahisi kueleweka na vya kusaidia. Tafadhali angalia mpangilio wake wote kabla ya kuujifunza au kuufundisha. Fomyula ya kujifunza vitabu vya Agano Jipya (4,1, 13,1,7,1) ni utunzi wake mwandishi.

Migawanyiko baadaye inavunjwa katika makundi ili kwamba wanafunzi waweze kusema ni kitabu gani wanajifunza. (Makundi haya yanajulikana vizuri katika ulimwengu wote wa Kibiblia.) Kwa mfano, Warumi ni barua ya kanisa, wakati ambapo I na II Timotheo ni barua za kichungaji. I Petro ni ya kundi la barua za watu wote. Kozi hii haikukusudiwa kutoa maelezo mapana juu ua kila kitabu. Badala yake, ni kukuwezesha kukumbuka kila kitabu kwa kupitia maneno machache, mstari wa mkuu, au kundi ambalo kinastahili kuwapo.

Wale ambao hufundisha kozi hii wanaweza kubadili vitu fulani katika kozi hii kama wanakielewa vizuri kitabu fulani na wana njia nyingine za kuelezea mawazo yake kiujumla. Kozi hii haikuvuviwa lakini mwandishi amefanya kazi kubwa ili kuifanya ya kueleweka na amejitahidi kuwa katika usahihi katika ujumbe wa kiujumla wa kitabu.

## **Wazo linalotawala la Agano Jipya ni:** KUTIMILIKA

Agano la Kale lilikuwa na:

- Sikukuu zisizokuwa na maelezo
- Makusudi yasiyofikiwa
- Shauku ambazo hazikukidhiwa
- Nabii ambazo hazikutimilika

**Katika Agano Jipya, Kristo anatimiliza yote haya.**

*Wafanye wanafunzi wako warudie namba hizi mpaka wajue zinawakilisha vitabu gani. Kisha, watake wazikariri ili waweze kuvijua vitabu vya Agano Jipya katika makundi.*

### Vitabu vya Agano Jipya

Injili 4
Kitabu 1 cha Historia
Nyaraka 13 Zilizoandikwa na Paulo
Mwandishi 1 Asiyejulikana
7 vya Waandishi Wengine
Kitabu 1 cha Unabii

### Injili 4

Mathayo
Marko
Luka
Yohana

### Kitabu 1 cha Historia

Matendo ya Mitume

### Nyaraka 13 Zilizoandikwa na Paulo

Warumi
I na II Wakorintho
Wagalatia
Waefeso
Wafilipi
Wakolosai
I na II Wathesalonike
I na II Timotheo
Tito
Filemoni

**Mwandishi 1 Asiyejulikana**

Waebrania

**7 vya Waandishi Wengine**

Yakobo
I na II Petro
I, II, na III Yohana
Yuda

**Kitabu 1 cha Unabii**

Ufunuo

**Migawanyiko mingine ya Nyaraka kimakundi**

Nyaraka za Kanisa
Nyaraka za Kichungaji
Nyaraka za Watu Wote

**Nyaraka za Kanisa**

Warumi
I na II Wakorintho
Wagalatia
Wafilipi
Waefeso
Wakolosai
I na II Wathesalonike

**Nyaraka za Kichungaji**

I Timotheo
II Timotheo
Tito

**Nyaraka za Watu Wote**

Filemoni
Waebrnia
Yakobo
I na II Petro
I na II na III Yohana
Yuda

# Tukirudi Mwanzoni:

## Injili 4

Mathayo

Kristo anaonyeshwa kama Mfalme

Marko

Kristo anaonyeshwa kama mtumishi

Luka

Kristo anaonyeshwa kama Mwana wa Adamu

Yohana

Kristo anaonyeshwa kama Mwana wa Mungu

Mathayo, Marko, na Luka
(Muhtasari wa Injili)

Injili hizi huonyesha zile kweli za nje za maisha ya Bwana na zile nyanja za kibinadamu za maisha ya Bwana.

Kwa sehemu kubwa, hotuba Zake za hadharani zimetolewa.
Galilaya ndipo mahali ambapo sehemu kubwa ya matukio hutokea.

Yohana
Huonyesha kweli za ndani za maisha ya Bwana pamoja na nyanja za kiungu za maisha Yake zikionyeshwa kwa uwazi zaidi.

Hotuba za faraghani ndizo zinazoelezwa kwa sehemu kubwa.

Matukio mengi yalitendeka Yudea.

# Mathayo (Sura 28)

**Mfalme**: uzao wa kifalme (Mbari ya Daudi)
Inaonyesha vizazi (1:1-17)

Mstari Mkuu: Mathayo 16:21

Hakuna ajuaye kwa uhakika ni lini kiliandikwa, lakini yawezekana mwishoni mwa miaka ya 50 au mwanzoni mwa miaka ya 60 B.K.

Ni simulizi ya Yesu wa Nazareti ambaye anatupatia ushahidi wenye ushawishi ya kuwa Yeye ndiye Masihi. Yeye ndiye ambaye ameuleta Ufalme wa Mungu hapa duniani na Yeye ndiye Mfalme! Anatimiliza ahadi ya Mungu ya Amani ya kweli na ukombozi kwa Wayahudi na Mataifa.

Mada kuu ambazo Mathayo anaonyesha ni:

Lile daraja kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Anatimiliza hili kupitia vizazi vyake (1:1-17), kutimia kwa unabii wa Agano la Kale (2:13-23), na usemi Wake kwamba ameitimiliza ile sheria, sio kuitangua (5:17-20).

Anaifikisha kazi yake ya kuokoa kwa watu wote (10:5-6, 28:19)

Kanisa kama jamii mpya ya imani likahamasishwa kushinda mipaka ya kikabila na tamaduni na kutafuta umoja. (11:28, 16:18-19, 28:19)

Kanisa lina uwepo wa Kristo unaoendelea na limepewa agizo kuu. (16:18, 18:15-20, 22:10, 28:19-20)

Kuna hotuba tano ambazo zaweza kuitwa mafundisho, au masomo, kuhusu kuwa mwanafunzi. Yapo katika Sura 5-7, 10, 13, 18-20 na 24-25.

**Yesu ni Mfalme wetu.**

# Marko (Sura16)

**Mtumishi:** simulizi iliyojaa matendo (maneno yanayomaanisha "papo hapo" au "mara moja" yanatumiwa mara kwa mara)
Hakionyeshi ukoo

Mstari Mkuu: Marko 10:45

Huenda kiliandikwa kati ya katikati au mwishoni mwa miaka ya 50 B.K. Uanafunzi (kama inavyoonekana katika mfano wa Kristo kama mtumishi) ndilo kusudi kubwa la kitabu. Ushirika na Kristo ndio moyo wa maisha ya mwanafunzi. Uanafunzi kwake humaanisha kumtegemea Yeye, kumkiri Yeye, kuyafuata mafundisho yake, kutazama tabia yake, na kufinyangwa na uhusiano wetu na Yeye. Ni pamoja na uzoefu wetu wa kukataliwa kama na yeye pia amepitia hayo.

Marko anatuonyesha:
Yesu ni mtu (1:25, 34, 44; 3:12, 4:10-12 na mahali kwingineko.)

Yeye ni mwana wa Adamu ambaye anazo nguvu zote na mamlaka lakini atalazimika kuteseka.
(1:6-34, 2:3-12, 23-28, 3:11, 5:7, na mahali kwingineko.)

Yeye ni Mwana wa Mungu (1:11, 3:11, 5:7, 12:6-8 na mahali kwingineko,)

Yesu ni Bwana (2:28, 12:35-37, 14:62)

Yesu anawaita wafuasi wake wamuige. (8:34-38, 9:35-37, 10:35-45)

Mstari mkuu 10:45 unasema: "Kwa maana Mwana wa Adamu naya hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."

Yesu, ambaye ni Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, na Ambaye ni Bwana anatuonyesha:

**Namna ya kuwa mtumishi.**

# Luka (Sura 24)

**Mwana wa Adamu**: huonyesha mwanzo Wake, maandalizi Yake, huduma Yake, mateso Yake, ushindi Wake
Huonyesha ukoo (3:23-38)

Mstari Mkuu: Luke 22:42

Kiliandikwa mnamo kama 62 B.K.
Luka alitaka watu wote wajue ya kuwa Injili ya Yesu ni kwa ajili ya watu WOTE. Anatafiti na kuandika ule ukweli wa tamaduni za Kikristo ambazo wasomaji wake wamefundishwa, hivyo wanajua ni za kweli. Pia watajua ya kwamba kwa kumuamini Yesu watapokea Roho Mtakatifu. Kwa kuwa Luka alikuwa tabibu, anatoa maelezo mengine mengi kuhusiana na kuzaliwa na kufa na yote yaliyoko katikati, kutoka katika mtazamo wake wa kisomi.

Muhtasari wa msingi unahusisha:
Miaka ya mwanzo ya Yesu (1:5-2:52)

Maandalizi ya Yesu kwa ajili ya huduma (3:1-4:15)

Huduma ya Yesu Galilaya (4:16-9:50)

Safari ya Yesu kwenda Yerusalemu (9:51 to 19:27)

Huduma ya Yesu Yerusalemu (19:28 to 21:38)

Mateso ya Yesu na kifo (22:1-23:56)

Kufufuka kwa Yesu (24:1-53)

**Yesu ni mwana wa Adamu.**

*Jina ambalo Yesu analipendelea zaidi kwa ajili Yake lilikuwa "Mwana wa Adamu". Limetajwa kama mara 78 katika Injili zote nne. Zinaweza kuwepo sababu kadha wa kadha kwa jambo hili. Inawezekana ni kwa sababu aliwakisha ubinadamu kamili, Alijifananisha na wale watu aliokuja kuwaokoa. Pengine lilimuunganisha Yeye na maisha yake ya duniani na mkazo wake katika ubinadamu Wake.*
*Hata hivyo, Mwana wa Adamu lilikuwa na pia ni uteuzi wa cheo cha ki-Masihi. Hii inatoka katika nukuu ya Danieli 7: 13-14. "…na tazama mmoja aliye mfano wa mwana wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbinguni akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu Naye. "Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake usioweza kuangamizwa."*

*Maeneo mengine machache ambako amlitumia hilo jina yalikuwa:*

*"Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kussameha dhambi' –hapo amwambia yule mwenye kupooza-- "Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyummbani kwako." (Marko 2:10)*

*“Kwa kuwwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.” (Luka 19:10)*

*“Akaanza kuwafundisha kwamba imempasa Mwana wa Adamu kupatikanan na mateso mengi, na kukataliwa na wazee, na wakuu wa makuhani, na kuuawa, na baada ya siku tatu kufufuka. (Marko 8:31)*

*“Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu Wake, na malaika watakatifu wote pamoja Naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu Wake,” (Matt. 25:31)*

*Kuna maeneo mengine mengi yenye rejea ya “Mwana wa Adamu” katika mstari. Jina hili halikuwahi kutumiwa na wanafunzi wake Kwake, lilitumiwa tu na Yesu kwa ajili Yake mwenyewe.*

## Yohana (Sura 21)

**Mwana wa Mugnu:** Kila sura huzungumza kuhusu uungu Wake
Hakionyeshi ukoo

Mstari Mkuu: Yohana 20:30-31

Pengine kiliandikwa wakati fulani kati ya 70 na 100 B.K. (wakati Yohana alipokufa)

Mada ya Injili ya Yohana fupi. Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa, Mwana wa Mungu.
Wote wale watakaomwamini watapata uzima wa milele!

Muhtasari mfupi:
Yesu, Neno lililofanyika mwili, (1:1-18)

Ishara ya kuwa Yeye ndiye Masihi (1:9-12:50)

Ushuhuda wa Yohana Mbatizaji

Huduma yake katika Yerusalemu, Yudea, Samaria na kwa Mataifa.

Upinzani Wake kutoka kwa Wayahudi

Pasaka ya mwisho

Kukataliwa Kwake na Wayahudi

Hotuba yake ya kuaga na simulizi ya wiki ya mateso (12:1-20:31)

Hotuba za Yesu kwa wanafunzi Wake katika Chakula cha Mwisho

Kukamatwa Kwake, hukumu, kifo na kuzikwa

Kufufuka Kwake, kuonekana, na kuwatuma wanafunzi wake
Mstari Mkuu ni 20:30-31

Mazungumzo ya mwisho na Petro, kumrejesha (21:1-25)

**Yesu ni Mwana wa Mungu.**



# *Kitabu 1 cha Historia*

## Matendo ya Mitume (Sura 28)

Matendo ya mitume na Roho Mtakatifu na kuanzishwa kwa kanisa la kwanza

Yesu Kristo kama Bwana aliye hai ndani ya maisha ya waaminio. Neno kuu ni shahidi!

Mstari Mkuu: Matendo 1:8

Pengine kiliandikwa mnamo wakati ule ule kama Injili ya Luka: 62 B.K.

*(Angalia muhtasari wa maisha ya Paulo chini)*

Muhtasari mfupi wa kitabu:
Yesu anawaandaa wanafunzi wake, anapaa, nafasi ya Yuda kujazwa, na Roho siku ya Pentekoste (1:1-2:13)

Matendo katika Yerusalemu (2:14 -5:42)

Matendo nje ya Yerusalemu (6:1- 12:25)

Matendo katika Kipro na Galatia ya kusini (13:1-14:28)

Baraza la Wayahudi (15:1-35)

Matendo katika Uyunani (15:36 -18:22)

Matendo katika Efeso (18:23-21:16)

Kukamatwa kwa Paulo Yerusalemu (21:17-23:35)


Paulo katika Kaisaria (24:1-26:32)

Ushuhuda wa Paulo katika Rumi (27:1-28)

**Roho analianzisha Kanisa Lake**.

## MATUKIO MAKUU YA MAISHA NA HUDUMA YA PAULO

- Kuzaliwa Tarso katika Kilikia (Matendo 21:39; 22:3)
- Mafunzo katika Yerusalemu (Matendo 22:3; angalia pia 26:4-5)
- Kuteswa kwa Kanisa la Kwanza (Matendo 8: 1-3; 9:1-2; 22:4-5; 26:9-11)
- Kuokoka (Matendo 9:3-19; 22:6-16; 26:12-18)
- Muda katika Arabuni, Dameski (Matendo 9:19-25; II Wakorintho 11:31-33; Wagalatia 1:17)
- Safari ya Yerusalemu (Matendo 9:26-29; Wagalatia 1:18)
- Kurudi Tarso (Matendo 9:30)
- Kufundisha katika Antiokia katika Siria (Matendo 11:25-26)
- Kupeleka msaada Yerusalemu kwa ajili ya njaa (Matendo 11:27-30; 12:25)
- Safari ya Kwanza ya Kimisheni (Matendo 13:1-14, 26)
- Huduma katika Antiokia (Matendo 14:26-28; 15:35)
- Baraza la Yerusalemu (Matendo 15:1-29)
- Safari ya Pili ya Kimisheni (Matendo 15:36-18:22)
- Safari ya Tatu ya Kimisheni (Matendo 18:23- 21:17)
- Kukamatwa Yerusalemu (Matendo 21:27-23:22)
- Kufungwa Kaisaria (Matendo 23:23-36, 32)
- Kuhamishwa Rumi (Matendo 27:1-28:15)
- Kufungwa nyumbani Rumi (Matendo 28:16-31)
- Kuachiliwa na Kuendelea na Safari (?) (angalia Tito 1:5; 3:12; I Tim. 1:3; 3:14; II Tim. 4:13, 20; pengine Warumi 15: 24,28)
- Kifungo cha Mwisho na Kifo Rumi (II Tim. 1:16-17; 4:6-8, 16-18)



# Nyaraka za Agano Jipya

***Kuwasaidia Wakristo Waishi kwa ajili ya Kristo Leo.***

Nyaraka za Kanisa ziliandikwa kwa makanisa. Nyaraka za Kichungaji ziliandikwa kwa wchungaji na nyaraka za kiujumla ziliandikwa kwa Wakristo wote. Hata hivyo, maandiko yote yafaa kwa mafundisho, kuonya na kuadibisha kwa waaminio wote (II Tim 3:16)

**Nyaraka 13 za Paulo**

**9 ni nyaraka za kanisa**

**3 ni nyaraka za kichungaji**

**1 ni waraka kwa watu wote**

## Warumi (sura 16)

Waraka wa kanisa kwa Wakristo walioko Rumi

Humueleza Yesu kama Haki yetu

Mstari Mkuu: Rum. 1:16-17

Pengine kiliandikwa mwaka 57 B.K.

Paulo anatoa mafundisho ya kitheolojia ya kiwango cha juu, ingawaje sio yote katika Rumi. Aina ya neno haki linatumika mara 55 katika kitabu hiki.

Baadhi ya mada…Mungu anawahukumu wote kwa sababu wote ni wenye dhambi, lakini pia anawapa wokovu kwa kupitia haki ya Mwana Wake. (1:18—3:20)

Sheri, ingawa ni njema, haiwezi kuishinda nguvu ya dhambi. (2:12-19)

Kuhesabiwa haki hupatikana kwa imani peke yake. (1:16-4:25)

Utukufu wa wakati ujao ni tumaini kwa wale wanaomtegemea Kristo. (5:1-8:39)

Mungu ni mkuu na, kupitia Kristo, anatimiza ahadi zake zote kwa Mataifa na Wayahudi sawasawa. Kila kitu kinafanywa kulingana na mpango Wake. (Rum 9:1-11:36)

Wakrito wanaitwa katika kuhudumiana, kuwa raia wema, kwenye utakatifu wa binafsi, na kuwapenda jirani. (12:1-13:14)

Mada hizi zinaweza kupatikana katika mistari mingine ya Warumi

**Yesu ndiye Haki Yetu**

# I Wakorintho (sura 16)

Waraka wa kanisa kwa Wakristo wa Korintho

Humuelezea Yesu Kristo, Atuunganishaye

Mstari Mkuu: I Kor. 15:3-5

Pengine kiliandikwa mnamo 53-55 B.K.

Kitabu hiki huzungumzia mada mbali mbali:

Paulo anataka waamini wenzake kufanya kazi kwa pamoja katika kupeleka ujumbe wa Injili. Wamegawanyika kutokana na kiburi cha baaadhi ya walimu wa Kikristo wenye nguvu zaidi, ambao hufundisha mafundisho potofu. Anawataka wawe na upendo na umoja ili kwamba nguvu ya Injili iweza kushuhudiwa kama hekima ya Mungu, na ujinga wa wanadamu uweze kuonekana (Sura 1-4).

Kuna maswala ya ndoa, talaka, chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu. Anazungumza kuhusu vitambaa vya kufunika kichwa na ibada sahihi kwa ujumla. Visitumike kuinua karama moja ya kiroho juu ya nyingine. Viwe na kazi ya kujenga imani ya walio dhaifu na kushuhudia sawasawa wasioamini. (Sura 5-14)

Sura mbili ambazo hukumbukwa mara kwa mara ni 13, sura inayohusu upendo, na 15, muhutasari wa kile ambacho Kristo amekifanya (15:3-5 ni mistari mikuu),

fikra kuhusu ufufuo wa wafu ziko katika Sura 15:12-58

**Yesu Kristo Ndiye Atuunganishaye**

# II Wakorintho (Sura13)

Waraka wa kanisa kwa Wakristo wa Korintho

Humuelezea Yesu Kristo, Utoshelevu wetu

Mstari Mkuu: II Kor. 12:9

Kiliandikwa mnamo 55-56 B.K.

Huu ulikuwa waraka wa Paulo ambao ulitoka nafsini mwake zaidi. Umejaa hisia za ushawishi na mifano inayoonyesha kwa nini yeye ni mtume wa Kristo na kwa nini ameteseka kihalali kwa ajili Yake. Mateso ya Paulo huonyesha kujitoa kwake kwa Kristo na sio kwa sababu ya kukosa ufanisi. Uvumilivu wake akiwa katika dhiki (aliyafanya yote katika shukrani na kutosheka) huonyesha nguvu ya ufufuo wa Roho. Paulo anawaambia Wakorintho ya kwamba ikiwa

watamkataa, wanamkataa Kristo mwenyewe kwa kuwa ujumbe wa Paulo, huduma na namna aishivyo ni umoja na Kristo. (Sura 1-6, 10:1-13:10)

Maswala mengine ambayo Paulo anayazungumzia ni nidhamu ndani ya kanisa na furaha ya wale wanaotubu, (Sura 6-7) na neema ya kutoa (Sura 8)

Sura 12 inatambulika kwa fundisho lake la jinsi neema ya Mungu inavyokamilishwa katika udhaifu. Yeye ni utoshelevu wetu!

**Tunamhitaji Yesu tu. Yeye ni utoshelevu wetu.**

## Wagalatia (Sura 6)

Waraka wa kanisa kwa Wakristo wa Galatia.

Humuelezea Yesu Kristo, Uhuru wetu

Mstari Mkuu: Gal. 5:1

Pengine kiliandikwa ama 47 au 48 B.K. na pengine ni moja kati ya nyaraka za kwanza za Paulo.

Kifo cha Kristo kimeleta agano jipya ili kwamba wanaomwamini wasilazimike kuifuata torati ya Kiyahudi. Ikiwa torati bado inahitajika, kuhesabiwa haki kwetu si kwa imani peke yake. Wafuasi wa Kristo sasa wapaswa kuishi kwa nguvu ya uongozi wa Roho Mtakatifu.

Kristo ametuweka huru kutoka katika kongwa la utumwa (5:1) hatuenendi tena kwa mwili (5:18-21) lakini kwa Roho anayetupatia tunda lake (5:22-25).

**Yesu anatufanya huru kwa njia ya imani peke yake.**

## Waefeso (Sura 6)

Waraka wa kanisa kwa Wakristo wa Efeso

Humuelezea Yesu Kristo, ambaye hufanya mambo yote kuwa umoja

Mstari Mkuu: Efe.1:7

Kiliandikwa mwaka 62 B.K.

Sura tatu za kwanza hueleza jinsi Kristo alivyoupatanisha uumbaji wote na Yeye nwenyewe na Mungu na jinsi ambavyo Yeye ndiye aliye mkuu. Sura hizi ni za kitheolojia. Sura tatu za mwisho hutoa maelekezo ya jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo.

Wokovu na neema kwa njia ya imani. (Sura 2)

Siri ya Injili na jinsi inavyounganisha Myahudi na Mmataifa. Pia, umoja na Amani ya Kristo. (Sura 3)

Mifano ya umoja wa mwili (Sura 4)

Maisha mapya katika upendo na kunyenyekeana (Sura 5-6)

Silaha zote za Mungu (Sura 6)

**Yesu hufanya mambo yote kuwa umoja.**

# Wafilipi (Sura 4)

Waraka wa kanisa kwa Wakristo wa Filipi

Humuelezea Yesu Kristo, Furaha yetu

Mstari Mkuu: Fil: 1:21-22 na Fil 4:8

Kiliandikwa 62 B.K.

Ujumbe mkuu wa Wafilipi ni kutia moyo. Paulo anaonyesha furaha yake ndani ya Kristo na jinsi ambavyo sisi nasi twapaswa kuwa nayo pia. Yuko gerezani wakati akiandika haya.

Mada nyinginezo…

Paulo anazungumzia kifungo chake na ni kwa jinsi gani kimeleta maendeleo katika Injili. Kwake Yeye kuishi ni Kristo na kufa ni faida. Tutateseka kwa ajili ya Injili (Sura 1)

Tunapaswa kuishi maisha ambayo yanawatanguliza wengine. Kristo ametuonyesha ni kwa namna gani tufanye hivyo. Tunapaswa kuishi kama nuru katika dunia na Paulo anatupatia mifano ya wengine ambao wamefanya hili. (Sura 2)

Paulo anasema hakuna cha kukilinganisha na kumjua Kristo. Tunapaswa kuufuata mfano huo. Haki inakuja kutoka kwa Kristo, si kutoka kwa wale wanaoipinga Injili. Sisi ni raia wa mbinguni. (Sura 3)

Tunapaswa kufurahi katika Bwana, tumpe Kristo fadhaa zetu katika maombi na tuwe chanya katika fikra zetu (Sura 4)

**Yesu Furaha Yetu licha ya mazingira.**

## Wakolosai (Sura 4)

Waraka wa kanisa kwa Wakolosai

Humuelezea Yesu Kristo, Uhai wetu

Mstari Mkuu: Kol. 2:6 na/au 3:4

Kiliandikwa mwaka 62 B.K. Paulo yuko gerezani wakati akiandika hiki.

Mada kuu ni Yesu Kristo ni Bwana juu ya uumbaji wote, unaoonekana na usionekana. Amewakomboa watu wake na amewaruhusu kushiriki katika mauti yake, kufufuka na utimilifu. Kristo ndiye aliye mkuu juu ya vitu vyote.

Paulo anaeleza Yesu ni nani katika Sura ya 1. Kisha anaonya dhidi ya mafundisho ya udanganyifu ambayo hutokea ndani ya kanisa (Sura 2). Fokasi iwe kwa Kristo na maisha yetu kule juu pamoja Naye (3:1-4) na jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo (3:5-4:6)

**Yesu ni ndiye Aliye Mkuu katika uhai wetu.**

## I Wathesalonike (Sura 5)

Waraka wa kanisa lililoko Thesalonike

Humuelezea Yesu Kristo, Yule Ajaye

Mstari Mkuu: I Thes. 4:15-17

Kiliandikwa wakati fulani kati ya mwaka 49-51 B.K.

Kurudi kwa Yesu Kristo kumetajwa katika kila sura ya kitabu hiki. (1:10, 2:19-20, 3:13, 4:13-18 na 5:1-11, 23-24.)

Mada nyingine ni…

Ghadhabu ya Mungu inakuja lakini si kwa ajili ya Wakristo (1:10, 5:4,9)

Wakristo wanapaswa kuishi maisha matakatifu (3:13, 4:3-8, 5:23) na wasikwepe wajibu wao wa kufanya kazi. (4:9-12, 5:14)

Kifo cha Yesu na kufufuka kwake ndio msingi wa tumaini la Mkristo. (4:14, 5:10)

**Yesu Ndiye ajaye karibuni.**

## II Wathesalonike (Sura 3)

Waraka wa kanisa lililoko Thesalonike

Humuelezea Yesu Kristo, Bwana wetu anayerudi

Mstari Mkuu: II Thes.2:3

Kiliandikwa baada tu ya I Wathesalonike 49-51 B.K.

Kuja mara ya pili kwa Bwana ndio ujumbe unaotawala kitabu hiki kama ulivyo katika I Wathesalonike. Hata hivyo, kitabu hiki kinaeleza jinsi ambavyo utakuwepo wakati wa ukengeufu (uasi) wa mtu aitwaye mtu wa kuasi, au mpingakristo, kabla ya kuja kwa Kristo. (2:3)

Kristo atakapokuja (2:8) Atamshinda na kuleta haki kwa Wakristo wanaokandamizwa. Ghadhabu itawajia watesi wao na kwa wasioamini kwa ujumla (1:5-10, 2:9-15)

Katika Sura ya 3, Paulo anaonya dhidi ya uvivu. Ikiwa mtu hatafanyakazi, na asile. Badala yake Wakristo wanapaswa kuuiga mwendo wa Paulo na Bwana. Wasichoke katika kutenda mema.

**Yesu atakuwa Bwana wetu anayerudi yote yatakapotimizwa.**

## I Timotheo (Sura 6)

Waraka wa Kichungaji

Uliandikwa kwa Timotheo, ambaye yuko Efeso

Humuelezea Yesu Kristo, Mwalimu wetu

Mstari Mkuu: I Tim. 4:12

Pengine kiliandikwa wakati fulani katika miaka ya kati ya 60 B.K.

Katika barua hii yote Paulo anasema kwamba Ukristo wa kweli unathibitishwa na mtindo wa maisha ya mwamini, ukiwa na misingi katika Injili. Viongozi wa kanisa wanapaswa kuongoza kwa mfano huu. Wazo la utaratibu mzuri wa kanisa katika kitabu ni kipengele kimojawapo cha wazo hili.

Timotheo:

Anapewa agizo la kukabiliana na walimu wa uongo katika Sura 1. Anatakiwa kuyatambua mafundisho ya uongo (4:1-5) na kuwakabili walimu wa uongo. (Sura 6) Yesu ndiye mwalimu wetu wa kweli.

Anapewa utambulisho wa maisha ambayo yamefinyangwa na Injili katika Sura ya 2 na 3.

Anaambiwa kwamba maisha yake yanapaswa kuwa ya mfano wa yale maisha yaliyofinyangwa na Injili (4:4-16)

Paulo anamuagiza Timotheo kwamba washirika wa kanisani waheshimiwe kwa kuzingatia umri na jinsia, wajane waheshimiwe, wazee na wakuu. (5-6:2)

**Yesu ndiye mwalimu wetu wa kweli katika maisha yetu na katika makanisa yetu.**

# II Timotheo (Sura 4)

Waraka wa Kichungaji

Uliandikwa kwa Timotheo kabla tu ya kifo cha Paulo, pengine wakati wa kifungo cha Paulo cha pili kule Rumi.

Humuelezea Yesu Kristo, mfano wetu

Mstari Mkuu: II Tim 4:2

Kiliandikwa mnamo kati ya 64 na 67 B.K.

Huu ni waraka wa Paulo ulio wazi wa kung’ang’ania katika Injili licha ya mateso. Wengine wamemwacha lakini anakumbuka kujitoa kwa Timotheo. (1:3-5) Waraka huu ni wa binafsi na nasaha kwa Timotheo kuendelea katika uaminifu wake kwa Kristo na mfano Wake.

Katika Sura ya pili anazungumzia tena kuhusu walimu wa uongo na anamtofautisha Timotheo na wao. Anayaelezea mafundisho ya uongo na kumhimiza Timotheo kufuata kilicho chema na kutojihusisha na hayo.

Anauelezea utauwa katika Sura ya 3 hasa katika nyakati za mwisho. Kisha anamkumbusha Timotheo kuhusu Neno lililovuviwa na jinsi lilivyo la msaada kwa waaminio.

Sura ya 4 anamuagiza Timotheo kuhubiri neno bila kujali wakati au mazingira kama ambavyo Paulo amefanya katika maisha yake yote. Ameteseka na anabashiri kifo chake karibuni.

**Yesu ni mfano wetu wa jinsi ya kuishi maisha yetu hapa.**

# Tito (Sura 3)

Waraka wa kichungaji ulioandikwa kwa Tito Krete

Humuelezea Kristo, kiolezo chetu.

Mstari Mkuu: Tito 3:4-5

Uliandikwa mnamo miaka ta katikati ya 60 B.K.
Paulo huenda yuko katika safari yake ya nne ya kimisheni kati ya kifungo chake cha kwanza na cha pili.

Mara nyingine tena, walimu wa uongo ni tatizo katika makanisa machanga. Tito aliachwa Krete ambako Paulo alikuweko, ili awasaidie wawe imara katika imani. Injili kama inavyoelezwa katika 3:3-7, inatumiwa kuonyesha tofauti kati ya mafundisho ya kweli na ya uongo.

Sura ya kwanza inaelezea sifa sahihi za mzee ukilinganisha na walimu wa uongo ambao wana tabia zilizo kinyume chake.

Paulo anamwambia Tito katika Sura ya 2 kufundisha mafundisho sahihi, kuyaishi, ili kwamba asiwepo atakayeuonea shaka uaminifu wake kwa Kristo au kudharau kile anachosema.

Sura ya 3 inamkumbusha Tito kuwa mtii kwa mamlaka na kuwa tayari kwa kila kazi iliyo njema. Anamkumbusha Tito jinsi ambavyo Kristo ametuokoa, si kwa sababu ya kile ambacho tumekifanya, lakini kwa rehema Zake. Paulo anasema kujihadhari na maswali ya upuzi na kujiepusha na wale wafanyao hayo. Wanachochea watu na kusababisha migawanyiko.

**Yesu ni kiolezo chetu cha namna ya kuwa kanisa na kuishi maisha yetu.**

# Filemoni (Sura 1)

Waraka wa Watu Wote

Humuelezea Yesu Kristo kama Bwana na Mkuu

Mstari Mkuu: Filemoni 10-11

Kiliandikwa mwaka 62 B.K.
Kitabu hiki chenye mistari 25 tu kinaonyesha ile nguvu ya Yesu Kristo inayosababisha mabadiliko katika maisha ya mtu. Onesimo amemkimbia bwana wake, Filemoni, ambaye ana kanisa nyumbani kwake. Akiwa amekwenda, Onesimo anakuwa Mkristo na anakuwa chini ya ulezi wa Paulo. Paulo anamsihi Filemoni kumpokea Onesimo kama ndugu mpendwa na mtendakazi pamoja naye. Onesimo si kwamba tu amepatanishwa na Mungu lakini pia anaweza kupatanishwa na bwana wake wa duniani.

**Yesu ni Bwana na Mkuu wetu**

# ***1 Mwandishi Asiyejulikana***

## Waebrania (Sura13)

Waraka kwa Watu Wote

Humuelezea Yesu kama mwenye kuwazidi wote, kuhani wetu mkuu na mwombezi wetu mbele ya kiti cha enzi.

Mstari Mkuu: Ebr. 4:12-16

Pengine kiliandikwa wakati fulani kabla ya mwaka 70 B.K. hakuna tarehe hasa inayojulikana.

Mada ni kwamba Kristo ni mkuu kuliko malaika ye yote, kuhani, au taasisi ya agano la kale. Haya hayana maana ukiyalinganisha na Kristo. Kwa hiyo, haina maana kufikiria kuyarudia. Kiliandikwa kwa Wakristo wa Kiebrania ambao walikuwa wamelijua Agano la Kale la Torati.

Muhtasari wa msingi ni:
Yesu ni mkuu kuliko malaika (1:1-2:18)

Yesu ni mkuu kuliko torati ya Musa (3:1 hadi 10:18)
Katika sehemu hii, Kristo anaonyeshwa kama kuhani mkuu aliye katika mfano wa Melkizedeki.
(4:12 hadi 8:13. Yeye ni mwombezi wetu katika kiti cha enzi mbinguni, (4:14-16)

Wito wa imani na uvumilivu unatolewa (10:19-12:29)

Manenno ya kuhitimisha (13:1-25)

Kitabu hiki ni hazina katika kuwatia moyo waaminio katika kushikilia imani yao.

**Yeye ni kuhani wetu mkuu, mwombezi wetu, na ni mkuu wa wote**

# ***Nyaraka 7 kwa Watu Wote zilizoandikwa na Waandishi Wengine***

## Yakobo (Sura 5)

Waraka kwa Watu Wote

(Yakobo ni kaka wa kambo wa kuzaliwa wa Yesu Kristo)

Humuelezea Yesu Kristo kiongozi wetu – uwe mtendaji wa Neno.

Mstari Mkuu: Yakobo 1:22

Pengine kiliandikwa mwanzoni mwa miaka ya 40 B.K.

Imani itajaribiwa (Yakobo 1:2-18)

Sikiliza na tenda Neno (Yakobo.1:19-27)

Dhambi ya upendeleo (Yakobo 2:1-13)

Imani bila matendo imekufa (2:14-26)

Kutiisha ulimu, hekima na udunia (3 hadi 4:12)

Dhambi za matajiri (4:13-5:12)

Maombi ya wale wenye imani (5:13-18)

**Yesu, ambaye ndiye Neno, ni kiongozi wetu katika kulitenda Neno.**

# I Petro (Sura 5)

Waraka kwa Watu Wote

Humuelezea Yesu Kristo ututkufu wetu ujao licha ya mateso ya hapa.

Mstari Mkuu: I Petro 1:3-4

Kiliandikwa mwaka 62 au 63 B.K.

Wokovu unatufanya tuwe wakimbizi hapa, lakini tuna urithi ujao (1:3-2:10)

Tunapokuwa tunaishi hapa kama watu Wake, tutamletea utukufu katika dunia hii iliyo adui: (2:11-4:11)
Tunapaswa kuvumilia katika mateso yetu (3:13-4:11)

**Yesu anatupatia utukufu ujao kule mbinguni, ingawaje tunaweza kuteseka hapa kwa ajili Yake.**

# II Petro

Waraka kwa Watu Wote

Humueezea Yesu chanzo chetu cha kuishi kiungu

Mstari Mkuu: II Petro 1:2-3

Pengine kiliandikwa wakati fulani kati ya mwaka 64-67 B.K.

Petro, ambaye ni shuhuda wa kuona kuhusiana na yale ambayo ameyaandika, anatuambia Kristo ni chanzo cha kuishi kiungu. (1:3-11)

Anayakumbusha makanisa kuishi maisha ya kiungu. Hili ni neno la kinabii kwao. (1:12-21)

Anawatathmini walimu wa uongo. (2:1-22)

Anaitamka Siku ya Bwana ijayo na ya kwamba itakuja kwa hakika. (3:1-13)

**Yesu ndiye chanzo chetu cha kuishi kiungu na kukaa katika njia licha ya uwepo wa walimu wa uongo.**

## I Yohana (Sura 5)

Waraka kwa Watu Wote

Huelezea kwamba Yesu ni upendo na nuru yetu

Mstari Mkuu I Yohana 5:13

Uliandikwa si baada ya miaka ya 90 B.K.

Mada tatu za msingi za maisha ya Kikristo ambazo Yohana anazitaja ni fundisho la kweli, maisha ya utii na kujitoa sana. Wale wanaomfuata Yeye wanaweza kuwashinda watenda maovu kwa sababu Yeye ndiye Nuru na mkuu kuliko roho yo yote ile ya mpingakristo iliyoko duniani.

Mungu ni Njia na Nuru (1-2:6)
Anatupatia sisi amri inayodumu katika dunia inayopita! (2:7-17)

Tunaweza kumshinda mpingakristo kwa kumkiri Mwana (2:18-3:10)

Tunaweza kuushinda uovu kwa kumsikiliza Yohana (3:11-4:6)

Tuna uhakika na Mungu kupitia upendo Wake (4:7-21)

Tunaweza kuwa na imani kwa Mwana kama njia ya uzima (5:1-12)

Imani na kuelewa (5:13-21)

**Yesu anatuonyesha sisi Yeye ni Upendo na ni Nuru ya njia yetu.**

## II Yohana (Sura 1)

Waraka kwa Watu Wote

Humuelezea Yesu kama kweli

Mstari Mkuu II Yohana mist. 1-2

Kiliandikwa wakati fulani kabla ya miaka ya katikati ya 90 B.K.

Mzee katika kitabu hiki anawaomba kanisa kuenenda katika kweli na katika amri ambayo Yesu aliwapa kutembea katika upendo. Anaonya kuhusu wadanganyifu na ya kuwa mmoja wao atakuwa mpingakristo. Anawaambia ya kwamba wale wanaodumu katika mafundisho ya Kristo wanaye Baba na Mwana. Msiyaamini mafundisho ya uongo ya mwingine ye yote.

**Yesu ni Kweli**

# III Yohana (Sura 1)

Waraka kwa Watu Wote

Humuelezea Yesu kama aliye mwema, na pia kweli

Mstari Mkuu III Yohana mst. 4

Kiliandikwa katika kipindi kimoja na I na II Yohana, kabla ya miaka ya katikakati ya 90 B.K.

Kiliandikwa kama waraka wa binafsi kwa Gayo. Yohana ana furaha, kwa kuwa mmoja wa watoto wake anaenenda katika kweli pamoja na upendo! Anamuagiza kuwasaidia watu ambao ni watendakazi wenzake katika ile kweli. Anasema usiwasikilize wale wanaoiiga kweli lakini ni waovu, kama vile Diotrefe. Ye yote afanyaye mema ametoka kwa Mungu.

**Yesu, ambaye ni Mwema, anatuonyesha jinsi ya kuenenda katika Kweli.**

# Yuda (Sura 1)

**Waraka kwa Watu Wote**

(Yuda ni kaka wa kambo wa kuzaliwa wa Yesu)

Humuelezea Yesu Kristo kama mtunzaji

Mstari Mkuu: Yuda 24

Kiliandikwa miaka ya katikati ya 60 B.K.

Yuda anawaambia watu kuishindania imani ya Yesu Kristo. Watahitajika kuvumilia pamoja na kuwepo kwa walimu wa uongo. Ni lazima wawaapinge, na Yuda anawakumbusha ya kuwa katika siku za mwisho watakuwepo wenye kudhihaki (mst 18), lakini pia anawakumbusha ya kuwa Yesu atawahifadhi wasijikwae na atawasimamisha bila mawaa, kama ilivyosemwa katika mstari mkuu (24)

**Yesu anawaita, anawapenda na kuwatunza watu wake milele**. (mst 1)

# ***Kitabu 1 cha Unabii***

## Ufunuo (Sura 22)

**Kiliandikwa na mtume Yohana**

Humuelezea Yesu Kristo kama Mfalme wetu mshindi

Mstari Mkuu: Ufu. 1:19
Pengine kiliandikwa mwaka 95 au 96 B.K.

Ufunuo si kitabu cha unabii tu lakini pia ni cha kitume, ikimaanisha kinayafunua mambo ambayo hatungeweza kuyajua kwa njia nyingine. Kimeandikwa kwa mtindo ambao ni wa kimafumbo. Kinaifunua vita ya kiroho isiyoonekana ambayo kanisa linapambana. Kinaonyesha mgogoro wa kiulimwengu ulioko kati ya Mungu, Kristo na Shetani na majeshi yake maovu. Kitabu kinalionya kanisa na kinatoa sababu za kanisa kupita katika mateso na kubaki likiwa safi kutoka katika maovu ya dunia yao inayojulikana. Kwa kuwa huu ni mtazamo wa kiujumla, muhtasari hapo chini ni mwongozo kwa ajili ya mwanafunzi kutumia na kuweka nyama katika hayo maelezo. Biblia nzuri yenye ufafanuzi kwa ajili ya kujifunzia itakusaidia.

Dibaji (1:1-8) inahusisha tangazo la kuja kwa Mfalme.

Mwili (1:9 hadi 22:5)

Hitimisho (22:6-21)

Muhtasari unachukuliwa kutoka 1:19:  mambo ambayo Yohana ameyaona (mst.1-20), mambo yaliyoko sasa (waliyoandikiwa makanisa 7, 2:1 hadi 3:29), na yale ambayo yatatokea (4:1-22:5).

Mwana Kondoo na gombo: (4:1-5:14)

Malaika na tarumbeta za tahadhari ya ghadhabu ijayo. ((8:2-11:18)

Mgogoro wa kiulimwengu kati ya Kristo na Shetani: unahusisha yule mwanamke, mwanawe, lile joka na wale wanyama (11:19-14:20)

Vitasa na ghadhabu ya mwisho ya Mungu (15:1-16:21)

Yule kahaba Babeli (17:1-19:10)

Kuangushwa na kushindwa kwa wanyama na joka, na hatimaye mauti (19:11-20:15)

Mambo yote yanakuwa mapya (21:1-22:5)

Hitimisho (22:6-21)

Hii inahusisha ahadi ya kwamba Yesu yuaja mapema, maonyo dhidi ya kukibadili kitabu na ahadi ya baraka.

Licha ya yale mapambano, ile migogoro, yale maonyo, ule udanganyifu,

## Yesu ndiye Mfalme wetu ashindaye milele!

### Amina na Amina!